

NGELI ZA NOMINO ZA KI-MICHEWENI¹

Hamad Khamis Juma

Ikisiri

Makala hii inachunguza na kuainisha ngeli za nomino katika Ki-Micheweni. Data iliyotumika katika makala hii imekusanywa kutoka uwandani kuanzia mwezi Januari hadi Machi, 2015. Uchambuzi na uwasilishaji wa data iliyotumika katika makala hii umeongozwa na Nadharia ya Mofolojia Asilia ya Dressler (1985). Nadharia hii hubainisha viambishi awali vya nomino na dhima zake kisemantiki. Matokeo ya uchunguzi huu yanabainisha kuwa Ki-Micheweni kina ngeli za nomino 18. Kwa kutumia mkabala wa viambishi awali vya nomino tumeweza kuainisha kwa kutenga viambishi vya nomino vya umoja na wingi katika ngeli tofauti katika uainishaji wa msingi. Hali kadhalika, katika uainishaji mdogo wa ngeli za nomino tumeona kuwa ngeli zenye mtawanyiko ni zile zinazohusu wanyama, sehemu za mwili na vitu visivyo hisivu. Aidha, tumebaini kuwa dhima za kisemantiki kama vile, ukubwa, tabia mbaya na dhuhaka zipo katika ngeli ya 5/6 na hali ya udogo, ubaya, uzuri zipo katika ngeli 7/8. Hapa tumebaini tofauti kati ya Ki-Micheweni na lugha nyingine za Kibantu. Kwa sababu Kahigi (2005) anaeleza kuwa dhima ya udogoshaji katika lugha za Kibantu zinapatikana katika ngeli ya 12/13 pekee.

1.0 Utangulizi

Makala hii inalenga kuainisha ngeli za nomino za Ki-Micheweni. Maandiko ya awali kuhusu sarufi ya Ki-Micheweni yalitolewa na Whitely (1958). Katika kitabu chake anagusia kwa uchache sana msamiati na miundo ya Ki-Micheweni. Khamis (1984), pia kwa muhtasari anaeleza sarufi ya Ki-Micheweni kwa kubainisha vipengele vya fonolojia, mofolojia, msamiati na miundo. Katika kazi zao wanaainisha ngeli za nomino za Kipemba na wala si Ki-Micheweni. Juma (2011) anajadili ngeli za Ki-Micheweni lakini uainishaji wake unafuata kigezo cha Khamis (1984). Hata hivyo, hakuna uchunguzi wa kina uliofanywa kuhusu ngeli. Kwa sababu hiyo uchunguzi huu unabainisha ngeli za nomino za Ki-Micheweni.

Makala hii imegawika katika sehemu zifuatazo, sehemu 1.0 ni utangulizi, sehemu 2.0 inawasilisha mkabala wa kinadharia, sehemu 3.0 inawasilisha uainishaji wa ngeli za nomino, sehemu 4.0 ni muhtasari wa uainishaji wa ngeli na sehemu 5.0 inatoa hitimisho.

2.0 Mkabala wa Kinadharia

Uchunguzi huu unaongozwa na Nadharia ya Mofolojia Asilia iliyopendekezwa na Dressler (1985). Nadharia hii hutumika kuainisha viambishi awali vya nomino na dhima zake kisemantiki. Pia, katika uchambuzi na uwasilishaji wa data ya makala hii, tumetumia mikabala mitatu sanjari na nadharia hiyo. Mikabala hiyo ni mkabala wa kimofolojia, mkabala wa kisintaksia na mkabala wa kisemantiki.

¹ Lahaja ndogo ya Pemba inayozungumzwa pembe ya Kaskazini Mashariki ya kisiwa cha Pemba.

Mkabala wa kimofolojia umetumika kuainisha viambishi awali vya umoja na wingi vya nomino. Hata hivyo, mkabala huu una udhaifu wake kwa sababu baadhi ya ngeli hufanana katika viambishi. Mfano, ngeli ya 1, 3 na 18 zina viambishi awali *mu-* (Kahigi, 2005). Hivyo ni vigumu kuutumia mkabala huu pekee. Mkabala wa kisintaksia, pia, umetumika kuweka vipatanishi vya kiima, yambwa na vivumishi katika sentensi. Mkabala huu nao una changamoto yake kwa sababu kuna vipatanishi vinavyofanana kwa baadhi ya ngeli.

Pia, tumetumia mkabala wa kisemantiki ambao huzigawa nomino kwa kigezo cha maana. Mkabala huu umetusaidia kuziweka pamoja nomino zenye maana zinazofafana au kukaribiana kwenye vikoa vya maana. Aidha, mkabala huu wakati mwingine unaleta utata wa uainishaji kwani maana za maneno hubadilika kulingana na mazingira ya kijiografia, matumizi ya lugha katika jamii na utamaduni (Massamba, 1995).

Kwa ujumla, katika uchunguzi huu tumetumia nadharia ya Mofolojia Asilia na mikabala ya kimofolojia, kisintaksia na kisemantiki. Nadharia na mikabala hiyo, imesaidia kwa kiasi kikubwa sana katika uchambuzi na uwasilishaji wa data.

3.0 Uainishaji wa Ngeli za Nomino

Uainishaji wa ngeli za nomino katika makala hii umebainishwa kwa njia mbili. Mosi, kwa kutumia kigezo cha uainishaji wa msingi. Huu ni mkabala unaozingatia mofolojia na sintaksia ambapo viambishi ngeli vya umoja na wingi na vile vya upatanisho wa kisarufi huzingatiwa. Pili, tumezianisha nomino kwa uainishaji mdogo wa ngeli za nomino. Katika uainishaji huu nomino zimeainishwa kwa kuzingatia dhima zake kisemantiki.

3.1 Uainishaji Kwa Msingi wa Ngeli za Nomino

Katika sehemu hii, tunainisha ngeli za nomino za Ki-Micheweni kwa kutumia mkabala wa kimofolojia na kisintaksia. Mkabala huu hutumika kuzigawa nomino katika makundi mbalimbali kwa kuzingatia viambishi vya nomino vya umoja na wingi pamoja na vipatanishi vyake katika sentensi (Kahigi, 2005). Ki-Micheweni kama kilivyo Kiswahili sanifu, muundo wa nomino hauna kiambishi kitangulizi badala yake huanza na kiambishi ngeli kikifuatiwa na shina la neno. Jedwali lifuatalo linaonyesha nomino na viambishi ngeli vyao na viambishi patanishi vyao vya kiima, yambwa na vivumishi katika Ki-Micheweni:

Jedwali na.1: Mfumo wa Ngeli za Nomino za Ki-Micheweni na Viambishi patanishi

Ngeli	KANg		Mf. Kipemba		Kiswahili		KK		KY		KV	
	U	W	U	W	U	W	U	W	U	W	U	W
1/2	n-/	wa-	<i>ntu</i>	<i>watu</i>	mtu	Watu	a-/ yu-	wa-	n/ m	wa	n-/ m-	wa-
	m-		<i>mvulyana</i>	<i>wavulyana</i>	mvulana	Wavulana						
	mu-		<i>muume</i>	<i>waume</i>	mume	Waume						
	mw-		<i>mwana</i>	<i>wana</i>	mtoto	Watoto						
3/4	n-/	mi-	<i>nti</i>	<i>miti</i>	nti	Miti	u-	i-	u	i	n-/ m-	mi-
	m-		<i>mpapai</i>	<i>miapai</i>	mpapai	Mipapai						
	mu-		<i>mwembe</i>	<i>miembe</i>	muembe	Miembe						
	mw-		<i>mwanzi</i>	<i>mi(y)anzi</i>	mwanzi	Mianzi						
5/6	ji-	ma-	<i>jimbi</i>	<i>majimbi</i>	jogoo	Majogoo	li-	ya-	li	ya	ø-	ma-
	ø-		<i>øfuti</i>	<i>mafuti</i>	goti	Magoti						
	i-		<i>ipu</i>	<i>mapu</i>	jipu	Majipu						
	zi-		<i>zicho</i>	<i>macho</i>	jicho	Macho						
7/8	ki-	vi-	<i>kiwatu</i>	<i>viwatu</i>	kiatu	Viatu	ki-	vi-	ki	vi	ki-	vi-
	ky-	vy-	<i>kyano</i>	<i>vyano</i>	chano	Vyano						
9/10	n-	n-	<i>nshi</i>	<i>nshi</i>	nchi	Nchi	i	zi	i	zi	n-	n-
11/10a	u	n	<i>ulimi</i>	<i>ndimi</i>	ulimi	Ndimi	u	zi	u	zi	n-	n-
12/13	*ka-	*tu-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-
14/6a	u-	ma-	<i>ugonjwa</i>	<i>magonjwa</i>	ugonjwa	Magonjwa	u-	ya-	u	ya	n-	ma-
15	ku-	ku-	<i>kuvyaa</i>	-	kuzaa	-	ku	-	ku	-	ku-	-
16	pa-	mwa-	<i>pahali</i>	mwahali	pahali	-	pa-	mu-	pa	mu	pa-	mu-
17	kwa-		<i>kwahali</i>		-	-	ku-		ku		ku-	
18	ma-		<i>mahali</i>		mahali	-	mu-		mu		mu-	

3.1.1 Ngeli ya 1/1a 2/2a

Ngeli hizi zinataja nomino ambazo zinahusu binadamu kwani nomino za ngeli hizi hurejelea majina ya watu. Ngeli ya 1 hubainishwa na kiambishi *mu-* na kiambishi awali cha ngeli ya 2 ni *wa-*. Hata hivyo, baadhi ya nomino za ngeli ya 1 hudondosha irabu *u-* katika kiambishi awali na kubakia na *m-/n-*². Pia iwapo shina la nomino litaanza na irabu, kiambishi ngeli kitakuwa *mw-*. Hivyo kiambishi awali cha ngeli ya 1 *mu-* kina alomofu {*m-/n-*, *mw-*}. Tuchunguze mifano ifuatayo:

² Utokeaji wa maumbo n-/m- hutegemea mazingira ya sauti, kwa mfano, katika Kipemba mahali pa sauti [m], inaposimama peke yake kama silabi katika neno, huwekwa sauti [n] mfano, ntu, nti, nk. Katika hali halisi nazali ya midomo [m] hubadilika kuwa nazali ya ufizi [n] kwa maneno yote ikiwa itafuatiwa na konsonanti isipokuwa konsonanti [p, b, f na v], mfano mvulana, mpapai, nk.

(1)

Ngeli 1		Ngeli 2	
<i>Nshikyana</i>	‘msichana’	<i>washikyana</i>	‘wasichana’
<i>Mvulyana</i>	‘mvulana’	<i>wavulyana</i>	‘wavulana’
<i>Mvyele</i>	‘mzee’	<i>Wavyele</i>	‘wazee’
<i>Muume</i>	‘mume’	<i>Waume</i>	‘waume’
<i>Mwana</i>	‘mtoto’	<i>Wana</i>	‘watoto’

Nomino za kundi hili zinarejelea watu wa kabila, kundi la kijamii, taifa au dini mahususi. Mifano:

(2)

<i>Ntumbatu</i>	‘Mtumbatu’	<i>Watumbatu</i>	‘Watumbatu’
<i>Muunguja</i>	‘Muunguja’	<i>Waunguja</i>	‘Waunguja’
<i>Mpemba</i>	‘Mpemba’	<i>Wapemba</i>	‘Wapemba’
<i>Muisilamu</i>	‘Muislamu’	<i>Waisilamu</i>	‘Waislamu’
<i>Nkirisito</i>	‘Mkristo’	<i>Wakirisito</i>	‘Wakristo’

Baadhi ya nomino za ngeli ya 1 na 2 zinatokana na mzizi wa kitenzi. Karibu nomino zote za aina hii huishia na kiambishi tamati cha nomino –*i* isipokuwa nomino chache za mkopo kutoka Kiarabu ambayo huishia na –*u*. Mifano:

(3)

<i>Nvyazi</i>	‘mzazi’	<i>Wavyazi</i>	‘wazazi’
<i>Mpisi</i>	‘mpishi’	<i>Wapisi</i>	‘wapishi’
<i>Mwandisi</i>	‘mwandishi’	<i>Wandisi</i>	‘waandishi’
<i>Muhasibu</i>	‘mhasibu’	<i>Wahasibu</i>	‘wahasibu’
<i>Nkarimu</i>	‘mkarimu’	<i>Wakarimu</i>	‘wakarimu’

Tukichunguza kwa makini tunaweza kubaini kuwa nomino hizi zinatokana na vitenzi elekezi.

Pia, nomino katika ngeli ya 1a zinarejea majina ya uhusiano wa familia na nomino nyingine ambazo hazichukui kiambishi awali³ badala yake hubainishwa na Ø- katika maumbo ya umoja na wingi. Tuangalie mifano:

(4)

<i>Mame</i>	‘mama’
<i>Dade</i>	‘dada’
<i>Kake</i>	‘kaka’
<i>shangazi</i>	‘shangazi’
<i>lahau</i> ⁴	‘kaka wa baba’

³ Baadhi ya nomino za familia katika ngeli ya 1 na 2 huchukua viambishi awali, mfano, *mkwe* – *wakwe*, *mjomba* – *wajomba*, *muamu* ‘mume wa ndugu’ – *waamu* nk.

⁴ Kaka wa baba katika familia au ukoo.

Kuna changamoto ambayo hujitokeza katika ngeli ya 1 na 2 kwa baadhi ya nomino zinazorejelea uhusiano wa familia. Kwa mfano, nomino *umbu* ‘ndugu wa jinsi tofauti’ wingi wake ni *maumbu*. Nomino hii haichukii viambishi awala (*m-*, *wa-*) wala (\emptyset -, \emptyset -) badala yake huchukua viambishi awali ngeli (\emptyset -,*ma-*) kutoka ngeli ya 5 na 6 na vivumishi vimilikishi ngeli ya 5 umoja na wingi katika ngeli ya 2. Lakini nomino hii huchukua viambishi vya upatanishi kutoka ngeli ya 1 na 2. Tuangalie mifano:

(5)

- (a) *Øumbu lyangu auka leyo*
ndugu yangu anaondoka leo
- (b) *Maumbu zangu wauka leyo*
Ndugu zangu wanaondoka leo

Mbali na nomino hizo kuna nomino za pekee ambazo hazirejelei majina ya watu lakini tunaweza kuziingiza katika ngeli ya 1 na 2. Mfano wa nomino hizo ni kama vile, *malaika*, *pepo* ‘shetani’, *muungu* ‘waungu’, nk

Upatanisho wa kisarufi wa ngeli ya 1 na 2 unabainishwa na mifano ifuatayo hapa chini:

(6)

- (a) *Nshikyana wangu nzuri aimba tarabu* (Ngeli 1)
‘Msichana wangu mzuri anaimba taarab’
- (b) *Washikyana wangu wazuri waimba tarabu* (Ngeli 2)
‘Wasichana wangu wazuri wanaimba taarab’
- (c) *Mwanangu nkubwa yuagonjwa mosi izi* (Ngeli 1)
Mtoto wangu mkubwa anaumwa siku hizi
- (d) *Wanangu wakubwa wagonjwa mosi izi* (Ngeli 2)
Watoto wangu wakubwa wanaumwa siku hizi
- (e) *Muume mbaya ampiga nkewe* (Ngeli 1)
‘Mume mbaya anampiga mke wake’
- (f) *Waume wabaya wampiga wake wawo* (Ngeli 2)
‘Waume wabaya wanampiga wake wao’

Kama tulivyoona katika jedwali na.1 hapo juu na katika mifano (6) (a) – (e) hapo juu tunabaini kuwa viambishi vya upatanishi vya ngeli ya 1 ni *yu-/a-* umoja na ngeli ya 2 ni *wa-* wingi. Pia, viambishi vya vivumishi ni *m-/n-* umoja na *wa-* wingi.

3.1.2 Ngeli 3 na 4

Ngeli hizi zinahusu majina ya mimea,, sehemu za mwili na nomino nyingine zisizohusu watu. Ngeli ya 3 hubainishwa na kiambishi awali *mu-* na ngeli ya 2 ni *mi-*. Hata hivyo, baadhi ya nomino za ngeli ya 3 hudondosha irabu *u-* katika kiambishi awali na kubakia

na *m-/n-*⁵. Pia iwapo shina la nomino litaanza na irabu, kiambishi awali kitakuwa *mw-*. Hivyo kiambishi awali cha ngeli ya 3 *mu-* ambacho kina alomofu {*m-/n-*, *mw-*}. Tuchunguze mifano ifuatayo:

(a) Majina ya miti na mimea:

(7)

Ngeli 3		Ngeli 4	
<i>nti</i>	‘mti’	<i>Miti</i>	‘miti’
<i>mpera</i>	‘mpera’	<i>mipera</i>	‘mipera’
<i>muwa</i>	‘mua’	<i>miwa</i>	‘miwa’
<i>muhogo</i>	‘mhogo’	<i>mihogo</i>	‘mihogo’
<i>mwembe</i>	‘mwembe’	<i>miembe</i>	‘miembe’

(b) Majina ya sehemu za mwili:

(8)

<i>nkono</i>	‘mkono’	<i>mikono</i>	‘mikono’
<i>muwili</i>	‘mwili’	<i>Miili</i>	‘miili’
<i>n’gongo</i>	‘mgongo’	<i>migongo</i>	‘migongo’
<i>nkiya</i>	‘mkia’	<i>mikiya</i>	‘mikia’
<i>n’domo</i>	‘mdomo’	<i>midomo</i>	‘midomo’

(c) Nomino nyingine mchanganyiko:

(9)

<i>nkoba</i>	‘mkoba’	<i>mikoba</i>	‘mikoba’
<i>nto</i>	‘mto’	<i>Mito</i>	‘mito’
<i>mpira</i>	‘mpira’	<i>mipira</i>	‘mipira’
<i>mwiba</i>	‘mwiba’	<i>Miba</i>	‘miiba’
<i>n’jusi</i>	‘mjusi’	<i>mijusi</i>	‘mijusi’

Upatanisho wa kisarufi wa ngeli ya 3 na 4 unabainishwa na mifano ifuatayo hapa chini:

(10)

(a) *Mpera* wangu *nkavu unku*gwa (Ngeli 3)
‘Mpera wangu **mkavu ume**anguka’

⁵ Utokeaji wa maumbo *n-/m-* hutegemea mazingira ya sauti, kwa mfano, katika Kipemba mahali pa sauti [m], inaposimama peke yake kama silabi katika neno, huwekwa sauti [n] mfano, ntu, nti, nk. Katika hali halisi nazali ya midomo [m] hubadilika kuwa nazali ya ufizi [n] kwa maneno yote ikiwa itafuatiwa na konsonanti isipokuwa konsonanti [p, b, f na v], mfano mvulana, mpapai, nk.

(b) *Mipera yangu mikavu inkugwa* (Ngeli 4)
‘Mipera yangu mikavu imeanguka’

(c) *N’ji nzuri unchafuliwa* (Ngeli 3)
‘Mji mzuri umechafuliwa’

(d) *N’ji nzuri unchafuliwa* (Ngeli 4)
‘Miji mizuri imechafuliwa’

Kama ilivyo katika jedwali na.1 na katika mifano (10) (a) – (d) hapo juu tunabaini kuwa viambishi vya upatanishi vya ngeli ya 3 ni *u-* na ngeli ya 4 *i-* ambapo viambishi vya vivumishi ni *m-/n-* na *mi-*.

3.1.3 Ngeli ya 5 na 6

Viambishi ngeli vya ngeli 5 ni *j-*, *Ø-*, *i-*, *zi-* na ngeli ya 6 ni *ma-*. Nomino za ngeli hizi zinahusu sehemu za mwili, matunda, bidhaa zinazozalishwa, majengo na nomino za maumbile asilia. Tuangalie mifano hapa chini:

(a) Majina ya sehemu za mwili:

(11)

Ngeli 5		Ngeli 6	
<i>zicho</i>	‘jicho’	<i>macho</i>	‘macho’
<i>Øfuti</i>	‘goti’	<i>mafuti</i>	‘mafuti’
<i>Øini</i>	‘ini’	<i>maini</i>	‘maini’
<i>Øshikiyo</i>	‘sikio’	<i>mashikiyo</i>	‘masikio’
<i>ipu</i>	‘jipu’	<i>Mapu</i>	‘majipu’

(b) Majina ya matunda:

(12)

<i>Ølimau</i>	‘limau’	<i>malimau</i>	‘malimau’
<i>Øpera</i>	‘pera’	<i>mapera</i>	‘mapera’
<i>Øpapayi</i>	‘papai’	<i>mapapayi</i>	‘mapapai’
<i>Ønanasi</i>	‘nanasi’	<i>mananasi</i>	‘mananasi’
<i>Øembe</i>	‘embe’	<i>maembe</i>	‘maembe’

(c) Majina ya bidhaa zinazozalishwa:

(13)

<i>Øgodoro</i>	‘godoro’	<i>magodoro</i>	‘magodoro’
<i>Økabati</i>	‘kabati’	<i>makabati</i>	‘makabati’
<i>Øziko</i>	‘seredani’	<i>maziko</i>	‘maseredani’
<i>Økoti</i>	‘koti’	<i>makoti</i>	‘makoti*’
<i>Øtenga</i>	‘susu’	<i>matenga</i>	‘masusu’

(d) Majina ya majengo:

(14)

<i>Ødaraja</i>	‘daraja’	<i>madaraja</i>	‘madaraja’
<i>Øjenzi</i>	‘jengo’	<i>majengo</i>	‘majengo’
<i>Øpaa</i>	‘paa’	<i>mapaa</i>	‘mapaa’
<i>Øjahazi</i>	‘jahazi’	<i>majahazi</i>	‘majahazi’

(e) Majina ya maumbile:

(15)

<i>Øvunde</i>	‘wingu’	<i>malimau</i>	‘malimau’
<i>iwe</i>	‘jiwe’	<i>mapera</i>	‘mapera’
<i>Øbonde</i>	‘bonde’	<i>mapapayi</i>	‘mapapai’

(f) Majina ya vimiminika yaliyo katika hali ya wingi tu huingia ngeli ya 6:

(16)

<i>maji</i>	‘maji’
<i>mate</i>	‘mate’
<i>maziwa</i>	‘maziwa’
<i>mafuta</i>	‘mafuta’

(g) Nomino nyingine zilizo katika hali ya wingi tu pia huingia ngeli ya 6:

(17)

<i>mashaka</i>	‘mashaka’
<i>malalamiko</i>	‘malalamiko’
<i>maskani</i>	‘maskani’
<i>masika</i>	‘masika’

Upatanisho wa kisarufi wa ngeli ya 5 na 6 unabainishwa na mifano ifuatayo hapa chini:

(18)

- (a) *zicho linaumiya*
‘**jicho limeumia**’
- (b) *macho yanaumiya*
‘**macho yameumia**’
- (c) *Ødaraja Øbovu lin’jengwa*
‘**Ødaraja Øbovu limejengwa**’
- (d) *madaraja mabovu yan’jengwa*
‘**madaraja mabovu yamejengwa**’

Kama ilivyo katika jedwali na.1 na katika mifano (18) (a) – (d) hapo juu tunabaini kuwa viambishi vya upatanishi vya ngeli ya 5 ni *li-* na ngeli ya 6 *ya-* ambapo viambishi vya vivumishi ni \emptyset - na *ma-*.

3.1.4 Ngeli ya 7 na 8

Viambishi ngeli vya ngeli ya 7 ni *ki-*, *ky-* ambapo ngeli ya 8 ni *vi-* na *vy-*. Nomino za ngeli hizi zinahusu vifaa au bidhaa zinazozalishwa, sehemu za mwili, lugha, watu wenye ulemavu. Tuangalie mifano:

(a) Majina ya vifaa:

(19)

Ngeli ya 7		Ngeli ya 8	
<i>kiti</i>	'kiti'	<i>Viti</i>	'viti'
<i>kiwatu</i>	'kiatu'	<i>viwatu</i>	'viatu'
<i>kikombe</i>	'kikombe'	<i>vikombe</i>	'vikombe'
<i>kyungu</i>	'chungu'	<i>vyungu</i>	'vyungu'
<i>kyano</i>	'chano'	<i>Vyano</i>	'vyano'

(b) Majina ya sehemu za mwili:

(20)

<i>kichwa</i>	'kichwa'	<i>vichwa</i>	'vichwa'
<i>kibipi</i>	'kiuno'	<i>Vibipi</i>	'viuno'
<i>kifuwa</i>	'kifua'	<i>vifuwa</i>	'vifua'
<i>kidole</i>	'kidole'	<i>Vidole</i>	'vidole'
<i>kisugudi</i>	'kisigino'	<i>visugudi</i>	'visigino'

(c) Majina ya jumuiya:

(21)

<i>kyama</i>	'chama'	<i>vyama</i>	'vyama'
<i>kyuwo</i>	'chuo'	<i>vyuwo</i>	'vyuo'
<i>kibeya</i> ⁶	---	<i>vibeya</i>	--
<i>kilobu</i>	'klabu'	<i>Vilobu</i>	'vilabu'

(d) Majina ya lugha na lahaja huingia katika ngeli ya 7:

(22)

<i>Kiswahili</i>	'Kiswahili'
<i>Kingereza</i>	'Kiingereza'
<i>Kifaransa</i>	'Kifaransa'
<i>Kimvita</i>	'Kimvita'
<i>Kipemba</i>	'Kipemba'

⁶ Kikundi cha watu wanaofanya kazi ya aina moja, mfano wavuvi

(e) Watu wenye ulemavu:
(23)

<i>kichaa</i>	'kichaa'	<i>vichaa</i>	'vichaa'
<i>kipofu</i>	'kipofu'	<i>vipofu</i>	'vipofu'
<i>kiziwi</i>	'kiziwi'	<i>viziwi</i>	'viziwi'
<i>kilema</i>	'kilema'	<i>vilema</i>	'vilema'
<i>kibubwi</i>	'bubu'	<i>vibubwi</i>	'mabubu*'

Nomino katika mfano (23) zinaibua changamoto katika uainishaji wake kwa nomino hizi kimofolojia zinazhukua viambishi ngeli vya ngeli ya 7 na ya 8. Lakini nomino hizi huchukua viambishi vya upatanishi, vivumishi na yambwa kutoka ngeli ya 1 na ngeli ya 2 kwa sababu nomino hizi zina sifa ya ubinadamu.

Upatanisho wa kisarufi wa ngeli ya 7 na 8 unabainishwa na mifano ifuatayo hapa chini:

(24)

(a) *kiwatu kizuri kinaibwa* (ngeli ya 7)
'kiatu kizuri kimeibiwa'

(b) *viwatu vizuri vinaibwa* (ngeli ya 8)
viatu vizuri vimeibiwa'

(c) *kisugudi kimpasuka* (ngeli ya 7)
'kisigino kimepasuka'

(d) *visugudi vimpasuka* (ngeli ya 8)
'visigino vimepasuka'

Kama ilivyo katika jedwali na.1 na katika mifano (24) (a) – (d) hapo juu tunabainikuwa viambishi vya upatanishi vya ngeli ya 7 ni *ki-* na ngeli ya 8 *vi-* ambapo viambishi vya vivumishi ni *ki-* na *vi-* pia.

3.1.5 Ngeli ya 9 na 10

Nomino za ngeli hizi zinahusu vifaa au bidhaa zinazozalishwa, vyakula na matunda, wanyama, ndege na nomino nyinginezo. Kiambishi ngeli cha ngeli ya 9 ni *n-* ambapo ngeli ya 10 ni *n-*. Kinachojibainisha katika ngeli hizi ni kwamba maneno mengi yasiyo maumbo ya umoja na wingi huingizwa humu. Tuangalie mifano:

(a) Majina ya bidhaa na vifaa;

(25)

Ngeli ya 9		Ngeli ya 10	
<i>sabuni</i>	'sabuni'	<i>sabuni</i>	'sabuni'
<i>nguwo</i>	'nguo'	<i>nguwo</i>	'nguo'
<i>shupa</i>	'chupa'	<i>shupa</i>	'chupa'
<i>simu</i>	'simu'	<i>Simu</i>	'simu'
<i>kamera</i>	'kamera'	<i>kamera</i>	'kamera'

(b) Majina ya vyakula na matunda:

(26)

<i>nyama</i>	‘nyama’	<i>nyama</i>	‘nyama’
<i>ndizi</i>	‘ndizi’	<i>Ndizi</i>	‘ndizi’
<i>shungwa</i>	‘chungwa’	<i>shungwa</i>	‘chungwa’
<i>shenza</i>	‘shenza’	<i>shenza</i>	‘shenza’
<i>nazi</i>	‘nazi’	<i>Nazi</i>	‘nazi’

(c) Majina ya maumbile:

(27)

<i>arizi</i>	‘ardhi’	<i>Arizi</i>	‘ardhi’
<i>pwaa</i>	‘bahari’	<i>Pwaa</i>	‘bahari’
<i>nshi</i>	‘nshi’	<i>Nshi</i>	‘nshi’
<i>panga</i>	‘pango’	<i>panga</i>	‘panga’

(d) Nomino dhahania:

(28)

<i>bahati</i>	‘bahati’	<i>bahati</i>	‘bahati’
<i>ndoto</i>	‘ndoto’	<i>Ndoto</i>	‘ndoto’
<i>ajali</i>	‘ajali’	<i>Ajali</i>	‘ajali’
<i>sifa</i>	‘sifa’	<i>Sifa</i>	‘sifa’

Upatanisho wa kisarufi wa ngeli ya 9 na 10 unabainishwa na mifano ifuatayo hapa chini:

(29)

(a) *Ndizi mbivu inliwa* (ngeli ya 9)

‘ndizi mbivu imeliwa’

(b) *Ndizi mbivu zinliwa* (ngeli ya 10)

‘ndizi mbivu zimeliwa’

(c) *sifa nzuri inamponza* (ngeli ya 9)

sifa nzuri imemponza

(d) *sifa nzuri zinamponza* (ngeli ya 10)

sifa nzuri zimemponza

Kama ilivyo katika jedwali na.1 na katika mifano (29) (a) – (d) hapo juu tunabaini kuwa viambishi vya upatanishi vya ngeli ya 9 ni *i-* na ngeli ya 10 *zi-* wakati kiambishi cha kivumishi ni *n-/m-*.

3.1.6 Ngeli ya 11

Ngeli ya 11 ina kiambishi ngeli *u-*. ngeli nyingi za kundi hili huchukua wingi kutoka ngeli ya 10 ambayo kiambishi ngeli chake ni *n-*. Ngeli hii inajumuisha ngeli zinazohesabika na zisizohesabika. Tuchunguze mifano:

(a) Nomino zinazohesabika zenye maumbo tofauti ya wingi:

(30)

Ngeli ya 11		Ngeli ya 10a	
<i>uso</i>	‘uso’	<i>nyuso</i>	‘nyuso’
<i>uzi</i>	‘uzi’	<i>nyuzi</i>	‘nyuzi’
<i>ulimi</i>	‘ulimi’	<i>ndimi</i>	‘ndimi’
<i>udevu</i>	‘udevu’	<i>ndevu</i>	‘ndevu’
<i>ubao</i>	‘ubao’	<i>mbao</i>	‘mbao’
<i>ubavu</i>	‘ubavu’	<i>mbavu</i>	‘mbavu’
<i>unywele</i>	‘unywele’	<i>nywele</i>	‘nywele’
<i>ufunguo</i>	‘ufunguo’	<i>funguo</i>	‘funguo’
<i>wembe</i>	‘wembe’	<i>nyembe</i>	‘nyembe’
<i>wimbo</i>	‘wimbo’	<i>nyimbo</i>	‘nyimbo’

(b) Nomino zisizohesabika ambazo hazina maumbo ya wingi:

<i>udongo</i>	‘udongo’
<i>ugali</i>	‘ugali’
<i>uji</i>	‘uji’
<i>ulimwengu</i>	‘ulimwengu’
<i>umeme</i>	‘umeme’
<i>unga</i>	‘unga’

Upatanisho wa kisarufi wa ngeli ya 11 unabainishwa na mifano ifuatayo hapa chini:

(31)

(a) *Uso mbaya unkwaruka* (ngeli ya 11)

‘uso mbaya umekwaruka’

(b) *Nyuso mbaya zinkwaruka* (ngeli ya 10)

‘nyuso mbaya zimekwaruka’

(c) *ufunguo n’digi unkwaga* (ngeli ya 11)

‘ufunguo mdogo umepotea’

(d) *funguo ndigi zinkwaga* (ngeli ya 10)

‘funguo ndogo zimempotea’

Katika mifano (31) (a) – (d) hapo juu tunabaini kuwa viambishi vya upatanishi vya ngeli ya 11 ni *u-* na ngeli ya 10a *zi-* wakati kiambishi cha kivumishi ni *n-/m-*.

3.1.7 Ngeli ya 14

Ngeli ya 14 ina kiambishi ngeli *u-*. Nomino dhahania zinazoundwa kutokana na nomino za makundi mengine huingizwa katika ngeli hii. Nomino nyingi za ngeli hii huundwa kutokana na mzizi wa kivumishi, nomino au kitenzi. Tuangalie mifano hapa chini:

(a) Nomino zinazoundwa kutokana na mzizi wa nomino:

(32)	<i>ujamaa</i>	‘ujamaa’	(< -jamaa)
	<i>utoto</i>	‘utoto’	(< -toto)
	<i>ufalume</i>	‘ufalme’	(< -falume)
	<i>urafiki</i>	‘urafiki’	(< -rafiki)
	<i>uzee</i>	‘uzee’	(< -zee)

(b) Nomino zinazoundwa kutokana na mzizi wa kivumishi:

(33)	<i>uhodari</i>	‘uhodari’	(< -hodari)
	<i>usafi</i>	‘usafi’	(< -safi)
	<i>uchafu</i>	‘uchafu’	(< -chafu)
	<i>uzembe</i>	‘uzembe’	(< -zembe)
	<i>upole</i>	‘upole’	(< -pole)

(c) Nomino zinazoundwa kutokana na mzizi wa kivumishi:

(34)	<i>upendo</i>	‘upendo’	(< -pend-)
	<i>uwezo</i>	‘uwezo’	(< -wez-)
	<i>ufufuo</i>	‘ufufuo’	(< -fufu-)
	<i>ungano</i>	‘ungano’	(< -unga-)

(d) Nomino zinazochukua wingi kutoka ngeli ya 6:

(35)	Ngeli ya 14	Ngeli ya 6a	
	<i>ugonjwa</i>	<i>magonjwa</i>	‘magonjwa’
	<i>uvuvi</i>	<i>mavuvi</i>	‘uvuvi’

Upatanisho wa kisarufi wa ngeli ya 14 unabainishwa na mfano wa 36 kama ifuatavyo:

(36)
(a) *Usafiwe unamponza* (ngeli ya 14)
‘usafi wake unamponza’

(b) *Ugonjwa mbaya unaingiya* (ngeli ya 14)
‘ugonjwa mbaya umeingia’

- (c) *Magonjwa mabaya yameingiya* (ngeli ya 6a)
 ‘magonjwa mabaya yameingia’

Katika mifano (36) (a) – (c) hapo juu tunabaini kuwa viambishi vya upatanishi vya ngeli ya 14 ni *u-*. Kwa baadhi ya nomino ambazo huchukua wingi kutoka ngeli ya 6a ni *ya-* ambapo kiambishi cha kivumishi ni *n-/m-* umoja na *ma-* wingi.

3.1.8 Ngeli ya 15

Ngeli ya 15 inahusu nomino zinazoundwa kwa kupachika kiambishi ngeli *ku-* katika shina la kitenzi. Mifano:

- (37)
kuvyaa ‘kuzaa’,
kuzinga ‘kutafuta’,
kucha ‘kuogopa’

Upatanisho wa kisarufi wa ngeli ya 15 unabainishwa na mifano ifuatayo hapa chini:

- (38)
 (a) *Kuvyaa sana kunanzeesa*
 ‘kuzaa sana kumemzeesha’
 (b) *Kuvyaa sana kunawazeesa*
 ‘kuzaa sana kumewazeesha’
 (c) *Kucha kwake kunamuokowa*
 ‘kuogopa kwake kumemuokoa’
 (d) *Kucha kwao kun’waokowa*
 ‘kuogopa kwao kumewaokoa’

Katika mifano (36) (a) – (d) hapo juu tunabaini kuwa kiambishi cha upatanishi na kivumishi vya ngeli ya 15 ni *ku-*.

3.1.9 Ngeli ya 16, 17 na 18

Ngeli ya 16, 17 na 18 katika Ki-Micheweni hubeba nomino za mahali. Ngeli hizi zimegawanyika katika makundi makuu mawili. Kuna nomino zinazojitegemea⁷ na nomino tegemezi⁸. Ngeli ya 16, 17, na 18 zinawakilishwa na viambishi ngeli *pa-*, *ma-/mu-*, *kwa-/ku* na wingi *mwahali*. Mfano:

- (39)
pahali ‘sehemu ambayo haikubainishwa.
mahali ‘sehemu iliyokaribu na imebainishwa na msemaji’
kwahali ‘sehemu iliyo mbali ya msemaji’
mwahali ‘wingi wa sehemu’

⁷ Zinaweza kusimama zenyewe kuonesha mahali na kuleta maana.

⁸ Haziwezi kusima zenyewe kuonesha mahali na kuleta maana.

Upatanisho wa kisarufi wa ngeli ya 16, 17 na 18 unabainishwa na mifano ifuatayo hapa chini:

(40)

- (a) *Pale pahali pachafu pansafiswa*
'Pale pahali pachafu pamesafishwa'
- (b) *Kule kwahali kuchafu kumesafiswa*
'Kule mahali kuchafu kumesafishwa'
- (c) *Mahali umu n'muchafu*
'Mahali humu ni muchafu'
- (d) *Mwahali mwao munfurika maji*
'mahali mwao mmefurika maji'

Katika mifano (40) (a) – (d) hapo juu tunabaini kuwa viambishi cha upatanishi na kivumishi vya ngeli ya 16, 17 na 18 ni *pa- mu- ku-* kwa mfuatano huo huo.

3.2 Uanishaji Mdogo wa Ngeli za Nomino

Katika sehemu hii, tunaelezea ngeli za nomino za Ki-Micheweni ambazo tumeziainisha kwa uanishaji mdogo wa ngeli za nomino. Kwa mujibu wa Massamba (1995) kuna uanishaji wa ngeli ambao huzingatia dhima za kisemantiki za nomino. Dhima kama vile, ukubwa, udogo, uzuri, ubaya, dharau, dhihaka na nyinginezo hujibainisha katika nomino baada ya kupachikwa kiambishi fulani cha nomino. Dhima hizo katika Ki-Micheweni zinabainishwa na kujadiliwa hapa chini:

3.2.1 Ukuzaji

Katika Ki-Micheweni dhima ya ukuzaji hujitokeza katika hali tofauti. Huingizwa katika ngeli ya 5 na kuchukua wingi katika ngeli ya 4. Kwa mujibu wa Kihore na wenzake (2001:121) ngeli ya 5/4 ni za nomino zihusuzo vitu vikubwa vyenye nguvu au kuogofya. Vitu vingine ambavyo maumbo yake yanaongezeka au nguvu zinapoongezeka na kuvifanya vitu hivyo visiwe vya kawaida basi huhamishiwa katika ngeli hizi. Mifano ifuatayo inabainisha:

(41)

- (a) *Joka limmiza kyura*
'Nyoka amemeza chura'
- (b) *Mijoka yammiza vyura*
'Nyoka wamemeza vyura'
- (c) *Jibwa lina njaa*
Mbwa ana njaa
- (d) *Mijibwa yana njaa*
Mbwa wana njaa

Pia, katika Ki-Micheweni dhima ya ukuzaji hufanywa kuonyesha hisia alizonazo msemaji kama vile; chuki, dhihaka, mzaha, wingi na hata kubainisha tabia mbaya au kitu kisichomvutia. Mifano:

- (42)
- (a) *Janajali zima halivijipika* (mzaha)
'Mwanamwari mzima hajui kupika'
 - (b) *Mijanajali mizima hayavijipiki* (mzaha)
'Wanawari wazima hawajui'
 - (c) *Juma fuga guruwe* (chuki)
'Juma anafuga nguruwe'
 - (d) *Juma wafuga miguruwe* (chuki)
'Juma wanafuga nguruwe'
 - (e) *Hilyo ndilyo jivi* (tabia mbaya)
'Huyo ndiye mwizi'
 - (f) *Hayo ndiyo mijivi* (tabia mbaya)
'Hao ndio wezi'
 - (g) *Nkutanoni kwena mijitu* (wingi)
'Mkutanoni kulikuwa na watu wengi'
 - (h) *Mikutanoni kwena mijitu* (wingi)
'Mikutanoni kulikuwa na watu wengi'

Mifano hiyo inaonyesha kuwa kuna vitu na wanyama kama vile mbwa, tumbili, nguruwe na kadhalika ambao Wapemba wa Micheweni hawawapendi kutokana na utamaduni wao. Wakati mwingine hutumia ngeli ya 5/4 kuonyesha hisia zao. Kwa ujumla tunaweza kusema kuwa dhima za kisemantiki katika nomino za Ki-Micheweni hutokana na sababu mbalimbali zikiwemo za kijamii na athari za kutoka nje.

3.2.2 Udogoshaji

Katika Ki-Micheweni pia baadhi ya nomino za ngeli mbalimbali hudogoshwa kwa kuingizwa katika ngeli ya 7/8. Tuangalie mifano hapo chini:

- (43)
- (a) *Kipaka kile kinlala* (udogo)
'Paka yule amelala'
 - (b) *Vipaka vile vinlala* (udogo)
'Paka wale wamelala'
 - (c) *Kijumba kile kin'jengwa lini?*
'Nyumba ile imejengwa?'

- (d) *Vijumba vile vimejengwa lini?*
'Nyumba **zile zimejengwa** lini?'

Mfano wa (43)(a) - (d) unabainisha kuwa nomino *kipaka* na *kijumba* zimehamishiwa katika ngeli hii ili kudogoshwa. Kupitia mifano hiyo tunabaini kuwa ngeli hii katika Ki-Micheweni ina dhima ya kisemantiki zaidi kuliko kisarufi.

3.2.3 Sifa Nzuri/Kupendeza

Ngeli ya 7/8 inahusu nomino za majina ya vitu vya kawaida kwa jumla, vitu visivyo na thamani na vifaa vya kutumia au kufanyia kazi (Kihore na wenzake, 2001:121). Katika Ki-Micheweni baadhi ya nomino zinazohusu watu au wanyama kutoka ngeli 1/2 wanaosifiwa kwa uzuri wa kuvutia au kupendeza huingizwa katika kundi hili. Tuchunguze mifano hapo chini:

- (44)
- (a) *Kijanajali kile nakipenda* (kupendeza)
'Mwanamwari **yule nampenda**'
 - (b) *Vijanajali vile navipenda* (kupendeza)
Wanawari wale nawapenda
 - (c) *Kitoto kidigi kyavijiwa pika* (sifa nzuri)
'Mtoto mdogo sana anajua kupika'
 - (d) *Vitoto vidigi vyavijiwa pika* (sifa nzuri)
'Watoto **wadogo** sana **wanajua** kupika'

Katika mfano wa (44) (a) - (d) tunabaini kuwa nomino *kijanajali* na *kitoto* zimehamishiwa katika ngeli hii si kwa kudharauliwa ila kwa sifa nzuri inayovutia au kupendeza.

3.2.4 Ushushaji Hadhi/Dharau

Katika Ki-Micheweni pia baadhi ya nomino za ngeli ya 1/2 zinazohusu watu au wanyama ambao wanadharauliwa na wenye tabia mbaya huingizwa katika kundi hili. Tuangalie mifano hapo chini:

- (45)
- (a) *Kizee kile kinaiba kuku* (tabia mbaya)
'Mzee **yule ameiba** kuku'
 - (b) *Vizee vile vinaiba kuku* (tabia mbaya)
'Wazee **wale wameiba** kuku'
 - (c) *Kijane⁹ kile kishakuwa cha kuoowa?* (kushusha hadhi)
'Mvulana **yule ameshakuwa** wa kuoowa?'

⁹ Mvulana aliyefikia baleghe.

(d) *Vijane vile vishakuwa vya kuoowa?* (kushusha hadhi)
 ‘Wajane **wale wameshakuwa** wa kuo?’

Katika mifano hiyo, (45)(a) - (d) inabainisha kuwa nomino *kizee* na *kijane* zimehamishiwa katika ngeli hii ili kudharauliwa au kushushwa hadhi kisaikolojia. Kupitia mifano hiyo tunabaini kuwa ngeli hii katika Ki-Micheweni ina dhima ya kisemantiki zaidi kuliko kisarufi. Pia, si ghalibu kusikia tungo kama hizo zikitumiwa katika Kiswahili sanifu.

4.0 Muhutajari wa Uanishaji wa Ngeli

Katika sehemu hii tunaeleze kwa ufupi mambo tuliyoyabaini katika ngeli za nomino za Ki-Micheweni. Katika uanishaji wa ngeli kimofolojia na kisintaksia tumebaini mambo yafuatayo:

4.1 Uingizaji wa Nomino za Mkopo

Maneno ya kigeni hasa yale ya mkopo huingizwa katika ngeli kwa kuzingatia umbo la nomino, upatamishi wa kisarufi na maana ya neno kisemantiki. Mfano:

(46)			
	1/2	<i>shetwani</i>	> kutoka Kiarabu (shaytwaan)
	5/6	<i>baseni</i>	> kutoka Kiingereza (basin)
	7/8	<i>kitabu</i>	> kutoka Kiarabu (kitaabu)
	9/10	<i>mutukari</i>	> kutoka Kiingereza (motor car)

Katika mifano 46 hapo juu, tunabaini kuwa baada ya kuangalia umbo la neno, neno hilo huingizwa katika ngeli kwa kuzingatia vipatanishi vyake kama vile kiima, yambwa, nk.

4.2 Uhamaji wa Ngeli

Baadhi ya lugha za Ki-Bantu zina unyumbufu wa ngeli, kwa maana kwamba baadhi ya nomino huhama kutoka ngeli moja kwenda nyingine. Pia, katika Ki-Micheweni baadhi ya nomino zina tabia ya kuhama kutoka kundi moja kwenda kundi jingine.

Katika Kiswahili sanifu nomino zote zihusuzo viumbe vyenye uhai na hisivu, zinaingia katika kundi 1/2. Lakini katika Ki-Micheweni kuna baadhi ya nomino ambazo huhamishiwa katika ngeli ya 9/10. Tuangalie mifano michache ifuatayo:

- (47)
- (a) *Ng'ombe in' chinjwa*
 ‘Ng'ombe amechinjwa’
 - (b) *Ng'ombe zin' chinjwa*
 ‘Ng'ombe wamechinjwa’
 - (c) *Nyuki in' niuma*
Nyuki ameniuma

- (d) *Nyuki zin'niuma*
'Nyuki wameniuma'

Mifano (47) inabainisha kuwa katika Ki-Micheweni kuna uhamishaji wa baadhi ya nomino za viumbe vyenye uhai na hisivu kutoka kundi la 1/2 (a – wa) kwenda kundi la 9/10 (i – zi). Hii inatokana na ukweli kwamba baadhi ya lugha za Ki-Bantu zina unyumbufu wa ngeli, kwa maana kwamba baadhi ya nomino huhama kutoka ngeli moja kwenda nyingine.

5.0 Hitimisho

Katika makala hii tumejaribu kuanisha na kujadili ngeli za nomino za Ki-Micheweni. Kwa kutumia mkabala wa viambishi awali vya nomino tumeweza kuainisha kwa kutenga viambishi vya nomino vya umoja na wingi kuwa katika ngeli tofauti. Uainishaji huu umesababisha kuwa na ngeli 18 kama zinavyoonekana katika jedwali na.1. Hali kadhalika, katika uainishaji mdogo wa ngeli za nomino tumeona kuwa ngeli zenye mtawanyiko ni zile zinazohusu wanyama, sehemu za mwili na vitu visivyo hisivu. Aidha, tumebaini kuwa dhima za kisemantiki kama vile, ukubwa, tabia mbaya na dhihaka zipo katika ngeli ya 5/6 na hali ya udogo, ubaya, uzuri zipo katika ngeli 7/8. Hapa tumebaini tofauti kati ya Ki-Micheweni na lugha nyingine za Kibantu kama vile Kisumbwa. MATHALANI, Kahigi (2005) anabainisha kuwa dhima ya udogo katika lugha za Kibantu zinapatikana katika ngeli ya 12/13 pekee lakini katika Ki-Micheweni dhima hiyo imejtokeza katika ngeli ya 7/8. Kwa kuhitimisha tunaweza kusema kuwa ngeli za nomino za Ki-Micheweni zina upekee hasa katika dhima za kisemantiki.

Marejeo

- Juma, H. K. (2011), "Tofauti za Kiisimu Baina ya Kiswahili cha Micheweni na Kiswahili cha Wete katika Kisiwa cha Pemba" (Tasnifu ya uzamili, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Kahigi, K. K. (2005), "The Sisumbwa Nouns: Its Classes and Derivation" . in *OCCASIONAL PAPER IN LINGUISTICS*. University of Dar es Salaam, LOT Project.
- Khamis, S. A. M. (1984), "Urban Versus Rural Swahili: A Study of Pemba Varieties". (Tasnifu ya uzamivu, haijachapishwa) Leipzig: Karl Marx University.
- Kihore, Y. M, D. P. B. Massamba na Y. P. Msanjila (2001), *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu (SAMAKISA): Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: TUKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Maho, J. F. (1999), *A Comparative Study of Bantu Noun Classes*. (Tasnifu ya uzamivu, haijachapishwa) Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Massamba, D. P. B (1995), "The Classification of Ci-Ruri Nouns". In *Journal of Asian and African Studies*. Nos 48-49, ILCAA. Tokyo University of Foreign Studies.
- Massamba, D. P. B. (2004), *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es salaam. TUKI: Chuo Kikuu cha Dar es salaam.

- Massamba, D. P. B., Y. M. Kihore na J. I. Hokororo (2001), *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu (SAMIKISA); Secundari na Vyu.* Dar es Salaam: TUKI. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Mohammed, M. A. (2001), *Modern Swahili Grammar.* Nairobi. East African Education Publishers.
- Polomé, E. C. (1967), *Swahili Language Handbook*, Center of Applied Linguistics, Washington DC.
- Whiteley, W. H. (1958), *The Dialects and Verse of Pemba.* Inter-territorial Language (Swahili) Committee.